

Malaria ni Hatari Zaidi kwa Wajawazito

Ugonjwa wa malaria ni hatari zaidi kwa mjamzito kwa sababu wakati wa ujauzito kinga ya mwili hushuka na kumweka mjamzito kwenye hatari ya kuugua malaria.

Mjamzito anaweza kuwa na vimelea vya ugonjwa wa malaria kwenye damu na asionyeshe dalili zozote za ugonjwa wa malaria kwakuwa vimelea vya ugonjwa wa malaria huwa na kawaida ya kujificha kwenye kondo la nyuma.

Madhara ya ugonjwa wa malaria wakati wa ujauzito

- Upungufu mkubwa wa damu
- Mimba kuharibika
- Mtoto kufia tumboni
- Kujifungua mtoto njiti
- Kuzaliwa kwa mtoto mwenye uzito pungufu

Namna ya kujikinga na malaria wakati wa ujauzito

Mjamzito anaweza kujikinga na ugonjwa wa malaria kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

- Ahudhurie kliniki ya wajawazito mara tu anapogundua ana ujauzito ili apewe dozi ya SP kuanzia wiki ya 14 na kila anapo hudhuria kituo cha kutolea huduma za afya, ilimradi dozi zipishane kwa wiki 4
- Mjamzito alale kwenye chandarua chenye dawa kila siku kwa kipindi chote cha ujauzito na baada ya kujifungua. Chandarua chenye dawa kinafukuza, kinaua, kinamuhakikishia usingizi mnono na kumpatia mjamzito kinga thabiti dhidi ya ugonjwa wa malaria
- Ni muhimu kwa mjamzito kwenda kwenye kituo cha kutolea huduma za afya kwa uchunguzi na tiba mara tu anapohisi dalili yoyote ya ugonjwa wa malaria

Mambo muhimu ya kuieleza jamii kuhusu malaria kwa wajawazito

- Ifahamishe jamii ni kwa nini wajawazito wako kwenye hatari zaidi ya kuugua ugonjwa wa malaria
- Watajije athari za ugonjwa wa malaria wakati wa ujauzito na namna ya kujikinga na ugonjwa wa malaria wakati wa ujauzito
- Sisitiza SP imethibitishwa kuwa ni salama kwa mama na mtoto aliye tumboni
- Wasisitize wanaume kuwa wanajukumu la kusaidia kuinga ugonjwa wa malaria wakati wa ujauzito.

Namna ya kusaidia wajawazito kujikinga na ugonjwa wa malaria

- Tembelea wajawazito wote walio kwenye jamii yako, jadiliana nao kuhusu namna ya kujikinga na malaria wakati wa ujauzito.
- Tembelea kliniki ya wajawazito kuangalia kama kuna SP kwa ajili ya wajawazito. Kama kituo cha afya hakina SP, jadiliana na uongozi wa jamii namna ya kuhakikisha kituo cha afya kinapata SP za kutosha.
- Wasisitize wanaume kuwa wanajukumu la kusaidia wenzi wao kujikinga na ugonjwa wa malaria wakati wa ujauzito. Kwa mfano kukumbusha tarehe ya kliniki au kuandaa usafiri wa kwenda kliniki
- Waelekeze maduka ya hati punguzo yalipo ili waweze kupata chandarua kwa bei ya punguzo
- Kama maduka ya vyandarua vya hati punguzo yako mbali sana, kwa kushirikiana na jamii andaa mkakati wakuwasaidia kuvifuata

Nenda Kliniki mapema



Pata Dozi mbili za SP



Lala kwenye chandarua chenye dawa kila siku



Malaria ni Hatari Zaidi kwa Wajawazito

Nenda Kliniki mapema



Pata Dozi za SP



Lala kwenye chandarua chenye dawa kila siku

